**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 01 Machi, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 – 2024/2025.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu Nam.10 ya 2009.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 – 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu Nam.10 ya 2009.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

108. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

Rais wa awamu ya tano na sita wa Tanzania kwa nyakati tofauti wameliagiza Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya DPP kuyatembelea magereza na kuzifuatilia kesi za muda mrefu ambazo zimekwama au zisizo na ushahidi wa kutosheleza, matokeo yake wapo watuhumiwa wengi sana kutoka magereza tofauti waliachiwa huru.

(a) Je, kwa magereza ya Zanzibar zoezi hilo limefanyika lini.

(b) Je, ni watuhumiwa wangapi wameweza kuachiwa huru kwa njia kama hizi na ni kutoka magereza yepi kwa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

3. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mashirika na baadhi ya Taasisi za Serikali Zanzibar hufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kutumia mfumo wa "*accrual basis"* badala ya "*cash basis"*.

Je, ni lini Mashirika na Taasisi zote za Serikali zitafunga hesabu zake kwa kutumia mfumo wa "*accrual basis"* ili kupatikana uhalisia wa hesabu za Taasisi hizo.

7. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Fedha zilizopatikana kupitia kodi ya miamala ya simu kwa upande wa Tanzania Bara zilitajwa hadharani na matumizi kuelezwa bayana, na tayari mafanikio kupitia huduma za afya na elimu pamoja na maji zimeanza kuonekana.

(a) Je, kwa upande wa Zanzibar fedha hizo ni kiasi gani zimepatikana na matumizi yake yameelekezwa wapi.

(b) Awali Zanzibar ilipata kiasi gani cha fedha hizo na mara baada ya kupunguzwa kwa kiwango cha tozo hizo kiasi gani kimeweza kupatikana.

(c) Kwa kuzingatia mabadiliko na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi. Je, Zanzibar inatarajiwa kupata kiasi gani kwa mwaka.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

75. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kojani kinatoa huduma kwa watu wengi zaidi ya matarajio yaliyokusudiwa. Na kwa kuwa watumishi wa kituo hicho ni wachache ukilinganisha na idadi ya watu wanaohudumiwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka katika kituo hicho wauguzi sita, watu wa madawa wawili, clinical officer mmoja na walinzi wawili.

141. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wananchi wengi, wakiwemo wa jimbo la Pandani, wamekuwa wakitilia mashaka uwezo wa Hospitali za Wete na Mkoani katika kuchunguza na kutibu maradhi ya moyo. Hata hivyo, kumekuwa na kesi za matokeo ya moyo kutanuka na kupelekea wagonjwa husika kupewa dawa kwa wingi hadi zinachosha na bila ya kupata maendeleo tarajiwa.

(a) Je, ni upi uwezo na utaalamu wa watendaji katika kuchunguza na kutibu maradhi ya moyo katika Hospitali za Wete na Mkoani.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuviongezea uwezo vitengo vya maradhi ya moyo vya Hospitali za Wete na Mkoani.

(c) Je, Serikali ina wataalamu bingwa wangapi wa maradhi ya moyo waliopangiwa kazi katika Hospitali za Wete na Mkoani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

8. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   Kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 188 pamoja na mambo mengine imeahidi kuhifadhi miundombinu ya michezo nchini, na kwa kuwa baadhi ya viwanja vinavyotumika kuchezea mpira vimeanza kuvamiwa na wananchi kwa matumizi mbali mbali.

   Je, ni lini Serikali itakihifadhi kiwanja cha mpira wa miguu cha ndugu Kitu kinachotumiwa na timu ya mpira ya Machomane United kwa kukizungushia uzio ili kuepusha uvamizi ambao unaendelea kujitokeza katika uwanja huo.

14. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   Katika hatua za kufufua mpira wa miguu kwa upande wa Zanzibar Serikali imekusudia kuvisaidia vilabu vya soka kiasi cha fedha kama sehemu ya kuvipa nguvu ya kukabiliana na changamoto mbali mbali.

   (a) Je, kwa vilabu vya daraja la kwanza (Premier) ni kiasi gani cha fedha kimekusudiwa kutolewa kwa kila kilabu.

   (b) Malengo halisi yaliyokusudiwa kwa matumizi ya fedha hizo ni yepi kwa vilabu hivyo.

   (c) Kuna masharti gani ya msingi yanayopaswa kutimizwa na vilabu husika kabla ya kupewa fedha hizo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

144. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

   Serikali inastahili pongezi kwa jitihada zake za kuongeza idadi ya skuli za maandalizi na msingi ili kuwafikia watoto wengi wa umri mdogo karibu na sehemu wanazoishi. Hata hivyo, maeneo ya Machengwe, Kivuugo na Mlindo ndani ya jimbo la Pandani yamekosa huduma hiyo pamoja na ukweli kwamba kuna watoto wengi wanaosoma kwenye mabanda yasiyostahiki kiusalama na kiafya za watoto au hakuna mabanda kabisa.

(a) Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi kuanzisha skuli za maandalizi na msingi za Machengwe, Kivuugo na Mlindo ndani ya jimbo la Pandani.

(b) Je, ni lini Serikali itawatambua walimu wanaojitolea kufundisha katika skuli za maandalizi na msingi za Machengwe, Kivuugo na Mlindo ndani ya jimbo la Pandani.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali kuhusu kuwapatia elimu watoto wenye umri mdogo wa Machengwe, Kivuugo na Mlindo wakati mpango wa uanzishwaji wa skuli za maandalizi na msingi za Machengwe, Kivuugo na Mlindo ukiendelea.

148. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na jitihada kubwa za Serikali katika kuimarisha mazingira na miundombinu ya kufundishia katika skuli. Hata hivyo, Serikali inaonekana kuzisahau skuli zote zilizomo ndani ya jimbo la Pandani kwa kuzikosesha madarasa stahiki na ya kutosha ya kusomea, ofisi na vyumba vya walimu pamoja na vyoo vya kutosha.

(a) Je, ni lini Serikali itayaongeza na kuyatengeneza madarasa ya kusomea ya skuli za msingi za Mzambarauni, Maziwani, Shengejuu, Pandani na Kiungoni.

(b) Je, ni lini Serikali itasaidia nguvu za wananchi za kuyaezeka upya mabanda yanayovuja na kuyaweka sakafu mpya mabanda ya skuli ya Mzambarauni.

(c) Je, ni lini Serikali itaongeza vyoo katika skuli zote zilizomo ndani ya jimbo la Pandani kutoka hali ya sasa ya wanafunzi 1,140 kwa vyoo vitano katika skuli ya msingi ya Mzambarauni na vyoo vitano kwa wanafunzi 1,496 katika skuli ya msingi ya Kiungoni.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

115. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Miongoni mwa vyanzo vikubwa vya mapato ya Shirika la Umeme (ZECO) ni kuongeza wateja.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea wateja baada ya kufanya malipo kuchelewesha kuungiwa umeme kwa wakati.

(b) Je, ni wateja wangapi walioungiwa umeme kwa mwaka 2020/2021.

160. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali inastahili pongezi kwa hatua inazochukua katika kusambaza na kuboresho mifumo ya usambazaji umeme nchini. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ndani ya jimbo la Pandani, kama vile Shengejuu ambavyo zamani viliunganishwa na umeme wa njia moja (single phase) ambao ulitosha ila kwa sasa miji imekuwa na inahitaji umeme wa njia tatu.

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa njia tatu ambao ndio unakidhi katika vijiji vingi vya jimbo la Pandani.

(b) Je, ni utaratibu upi unatumiwa na Serikali kutambua mahitaji sahihi na endelevu ya umeme katika kila kijiji.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kusambaza umeme stahiki na unaokidhi mahitaji mapya katika vijiji vya jimbo la Pandani.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

41. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Je, ni kwa kiasi gani maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ya mtandao “*internet*” yanasaidia ongezeko la uzalishaji na kukua uchumi wetu kwa kasi.

43. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha miundombinu ya Wakala wa Karakana Kuu ya Zanzibar kwa lengo la kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Wakala huyu amekuwa akilalamikiwa sana na taasisi na watu wanaoenda kupata huduma kituoni pale (Chumbuni) kutokana na uhaba wa wataalamu na ukosefu wa vifaa vya huduma muhimu zinazotarajiwa kupatikana kupitia kituo hiki.

(a) Je, tokea kuanzishwa kwa Wakala ya Karakana Kuu, Serikali imewahi kufanya tathmini na kujua faida na hasara inayopatikana kwa kuzingatia gharama kubwa iliyotumika katika kununua vifaa vya kisasa.

(b) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja kwa Wakala wa Karakana Kuu kuunganishwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ili kuimarisha utendaji na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

100. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika miaka hadi 2000, Shirika la ZSTC lilikuwa limejikita zaidi katika biashara ya karafuu na mbata. Hata hivyo baada ya kuanguka kwa zao la mbata ZSTC iliangalia upande mwengine wa kuanzisha viwanda vya mafuta ya miti na mimea mbali mbali.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Shirika hilo limeweza kupata tija kwa shughuli zake hizo mpya.

(b) Kwa kuwa kuwepo kwa zao la mbata ilikuwa ni msaada mkubwa kwa Serikali kuwa na viwanda vingi vya mafuta ya nazi, Je, Serikali kupitia ZSTC na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haiwezi kuanzisha mradi wa kufufua mradi wa zao la nazi ili kupata mbata za kutosha na kuanzisha viwanda vipya.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 – 2024/2025.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu Nam.10 ya 2009.

**Zanzibar,**
**01 Machi, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**